# Bajeti ya Elimu ya Mwaka 2016/2017
## Je, ni Kweli Imeongezeka?

Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali iliidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni 4,770 kwa matumizi ya sekta ya Elimu zikiwa zimejumuisha matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 22.1 ya jumla ya bajeti yote ya Taifa ambayo ni Shilingi Bilioni 29,539.6. Takwimu hizi hazijumuishi deni la taifa.

Kutokana na takwimu za matumizi ya sekta ya Elimu yaliyoidhinishwa, tunaweza kuona ongezeko la Shilingi Bilioni 882.3; kutoka Shilingi Bilioni 3,887 katika mwaka wa fedha wa 2015/16 hadi Shilingi Bilioni 4,769 kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 22.7

Hivyo kwa msingi wa mgawo wa bajeti iliyoidhinishwa, kuna ongezeko katika bajeti ya sekta ya Elimu, lakini mgawo halisi unahitaji kujadiliwa. Tazama Chati Namba1 hapa chini;

### Chati Namba 1: Bajeti ya Sekta ya Elimu – bila Deni la Taifa




*Chanzo: Bujeti ya Taifa 2015-16 & 2016-17*

Ni muhimu kuangalia kama bajeti iliyoidhinishwa inajumuisha deni la taifa au la kwa sababu deni la taifa huwa linapunguza bajeti inayoweza kutumika. Kwa mfano, kwa mujibu wa Bajeti ya Taifa Serikali imepanga kutumia Shilingi Bilioni 8,000 kulipia deni la Taifa kwa mwaka wa fedha wa 2016/17. Kiasi hiki hutolewa kutoka katika bajeti kuu na hivyo kusababisha matumizi ya bajeti hiyo kupungua nguvu. Kwa mfano, katika sekta ya elimu sehemu ya bajeti ya sekta iliyoidhinishwa dhidi ya bajeti ya taifa bila deni la taifa ni asilimia 22.1; kiwango ambacho si cha kuaminika. Lakini tukitoa malipo ya deni la taifa, sehemu ya bajeti ya sekta ya Elimu ikilinganishwa na bajeti ya taifa inakuwa sawa na asilimia 17 sawasawa kabisa na kiwango cha mwaka uliopita.

Chati zifuatazo zinalinganisha sehemu ya bajeti ya sekta ya Elimu dhidi ya bajeti ya taifa katika miaka miwili iliyopita kwa kuangalia matumizi yaliyoidhinishwa kabla na baada ya kutoa deni la taifa.

Chati Namba 2: Bajeti ya Elimu kama sehemu ya Bajeti ya Taifa (Pasipokuwa na Deni la Taifa)




Chati Namba 3: Bajeti ya Elimu kama sehemu ya Bajeti ya Taifa (Pamoja na Deni la Taifa)




*Chanzo: Bujeti ya Taifa 2015-16 & 2016-17*

Bajeti ya sekta ya Elimu hugawanywa tena katika bajeti ya kawaida na bajeti ya maendeleo. Katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2016/17 jumla ya Shilingi Bilioni 3,069.5, sawa na asilimia 64.3 zilitengwa kwa matumizi ya kawaida; wakati Shilingi Bilioni 1,700.5, sawa na asilimia 35.7 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Kimsingi sehemu ya bajeti ya kawaida ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo katika sekta ya Elimu inaonekana kuwa imeboreshwa na kukaribia uwiano unaopendekezwa wa walau 60:40 (Kawaida: Maendeleo). Kutokana na uchambuzi wa hapo juu uwiano wa mgawo katika mwaka 2016/17 ni 64:35 (kawaida: maendeleo). Uwiano unaendana na viwango vinavyotakiwa ukilinganisha na ule

wa mgawo wa mwaka uliopita wa 84:16. Chati ya chini inaonyesha uwiano huo:-

### Chati Namba 4: Mwenendo wa Mgawo wa Bajeti ya Sekta ya Elimu:- Kawaida dhidi ya Maendeleo




*Chanzo: Bujeti ya Taifa 2015-16 & 2016-17*

Kwa mujibu wa malengo ya bajeti na vipaumbele vilivyopangwa, lengo kuu la bajeti ya sekta ya Elimu katika mwaka 2016/17 ni kutekeleza elimu bure ya msingi kwa nchi nzima; kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; ujenzi; ukarabati wa miundo mbinu ya elimu; kuboresha thamani ya elimu kwa kujenga ujuzi unaotakiwa katika ngazi zote; kuimarisha Utafiti na Maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Kutekeleza na kufikia malengo haya yaliyopangwa; fedha za sekta ya elimu husambazwa kupitia Wizara zifuatazo ambazo hupokea kiasi tofauti kutegemeana na shughuli zinazofanyika:-

- Shilingi Bilioni 2,871.6 hupelekwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- Shilingi Bilioni 1,397 hupelekwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Shilingi Bilioni 500.1 hutengwa na Serikali kuu kupitia Wizara mbali mbali zinazoshughulika na elimu, yaani Wizara ya Wanawake, Jinsia na Maendeleo ya Mtoto na Wizara ya Afya na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

*Chati Namba 5: Mgawo wa Bajeti ya Sekta ya Elimu Ki-Wizara*




*Chanzo: Bujeti ya Taifa 2016-17*

Matumizi mengine muhimu kutokana na bajeti ya sekta ya elimu yanajumuisha Shilingi Bilioni 3,069.5 zilizopangwa kutekeleza "Mpango wa Elimu Bure ya Msingi"; ambapo Shilingi Bilioni 2,871.6 zimetengwa kama ruzuku za kuhawilishwa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA's). Shilingi Bilioni 197.89 hutengwa na Serikali kuu kupitia wizara mbali mbali. Mpango wa Mafunzo ya Teknolojia na Ufundi hupokea Shilingi Bilioni 44.61, Maendeleo ya sayansi na teknolojia hupokea Shilingi Bilioni 69.66; wakati Shilingi Bilioni 431.71 huenda katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi walioingizwa kwenye elimu ya juu na Bilioni 43.75 zitatumika kwa uhakiki wa thamani, ukarabati wa Vyuo vya Walimu, kuimarisha ukaguzi na kuanzisha Tume ya Huduma ya Waalimu (TSC).

## Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 2016/17

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni mshauri mkuu wa Serikali kuhusu mfumo wa elimu, hivyo hutoa miongozo kwa taasisi za elimu na mashirika yanayochangia katika malengo ya Serikali kuhusu elimu. Majukumu yake makuu ni kupanga mikakati, sera, na mipango ya mageuzi na maendeleo ya elimu; na kuandaa rasimu ya kanuni na taratibu, na kusimamia utekelezaji wake. Kufanikisha majukumu hayo Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia mwaka 2016/17 imeomba na kuidhinisha kutumia kiasi cha jumla ya Shilingi Bilioni 1,397 katika kugharamia ya shughuli za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2016/17.

Hili ni ongezeko la Shilingi Billioni 407.5, sawa na asilimia 41.2 kutoka Shilingi Bilioni 989.5 zilizoombwa na kuidhinishwa katika mwaka wa fedha wa 2015/16.

### Chati Namba 6: Jumla ya Mgawo wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia




*Chanzo: Bujeti ya Taifa 2015-16 & 2016-17*

Kati ya jumla ya Shilingi Bilioni 1,397, Wizara imepanga kutumia Bilioni 499.3 sawa na asilimia 35.7 ya jumla ya bajeti yote kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni pamoja na fedha kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na gharama nyingine. Hata hivyo, Wizara imetenga Shilingi Bilioni 897.7, sawa na asilimia 64.3 ya bajeti yote kwa matumizi ya maendeleo katika mwaka wa fedha wa 2016/17. Shughuli za maendeleo zinajumuisha ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu na miradi mingine chini ya wizara.

Wachambuzi wa bajeti na baadhi ya wadau wanafikiri kuwa uwiano baina ya bajeti ya kawaida na ya maendeleo ni mzuri sana; kwani juhudi nyingi zimeelekezwa katika matumizi ya ki-mtaji (maendeleo) kuliko matumizi ya kawaida.

*WEST-Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

### Chati Namba 7: Matumizi ya Wizara:  Kawaida Dhidi ya Maendeleo




*Chanzo: Bujeti ya Taifa  2015-16 & 2016-17*

Hata hivyo bajeti ya Wizara hugawanywa  tena katika matumizi ya  Bodi ya Mikopo na matumizi  mengine ya ki-mtaji  chini ya wizara. Kwa kugharamia elimu ya juu kupitia mikopo kwa wanafunzi walioingizwa katika taasisi za elimu ya juu, Serikali imetenga Shilingi Bilioni 431.71; hii ikiwa sawa na asilimia 31 ya jumla ya bajeti ya Wizara na asilimia 47 ya jumla ya bajeti ya Wizara kwa matumizi ya maendeleo, wakati Shilingi Bilioni 465.9 (sawa na asilimia 53) zimetengwa kwa ajili ya matumizi halisi ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2016/17.

### Chati Namba 8: Mgawo wa Fedha za Matumizi ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu




*Chanzo: Bujeti ya Taifa  2015-16 & 2016-17*

**Dondoo Muhimu za Kisera:**

- Bajeti zilizoidhinishwa zitangazwe baada ya kuzingatia deni la taifa kuepuka kutoeleweka kwa kuzingatia uwezo halisi wa matumizi ya bajeti ya mwaka husika. Mwaka 2016/17 bajeti iliyoidhinishwa haikujumuisha deni la taifa; hali hii ilifanya takwimu ya bajeti ionekane kuwa kubwa wakati hali halisi siyo kubwa kwa sababu sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa itatumika kulipa deni la taifa.

- Uwiano kati ya bajeti ya kawaida na ya maendeleo umeboreshwa na umekaribia kabisa uwiano unaopendekezwa wa 60:40. Tumeifurahia nia hii ya serikali na tunasisitiza kwamba iwe endelevu.

- Hata hivyo, bajeti ya Wizara kwa matumizi ya maendeleo bado imechangiwa gharama na kiasi cha fedha zilizojumuishwa kwa ajili ya huduma ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ambayo tunaiainisha kama matumizi ya kawaida.

- Mpango wa bajeti hauna uhusianao na mipango iliyopita kama vile Matokeo Makubwa Sasa ambayo kwao Serikali ilifanya umma kuamini kuwa ni mpango mzuri sana na unaofaa kuboresha elimu.

- Usambazaji wa bajeti ya sekta ya elimu kwa wizara mbali mbali kunapingana na misingi ya uwazi na uwajibikaji. Tunapendekeza kuwa sekta ya elimu iendeshwe na wizara moja au kwa kushirikiana na wizara moja tu yenye jukumu la Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs).

Kimeandaliwa na Hakielimu kwa niaba ya Kikundi Kazi cha Policy Forum cha Bajeti

POLICY FORUM
S.L.P 38486, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2780200/255 782317434
Baruapepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz